HOTUBA YA MHE. DKT HARRISON G. MWAKYEMBE (MB), WAZIRI WA MAMBO YA KATIBA NA SHERIA, KATIKA UFUNGUZI WA WIKI YA KUTOA HUDUMA KWA UMMA KATIKA KUADHIMISHA SIKU YA MAADILI NA HAKI ZA BINADAMU KITAIFA KATIKA VIWANJA VYA MNAZI MMOJA, DAR-ES-SALAAM
TAR. 05/12/2016

Mhe. Angellah Kairuki (MB), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora);

Mhe. George Masaju, Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

Kamishna Valentino Mlowola, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu;

Mheshimiwa Paul Makonda, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;

Dkt. Laurean Ndumbaro, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora);

Profesa Sifuni Mchome, Katibu Mkuu, Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria;

Profesa Mussa Assad, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG);

Dkt. Laurent Shirima, Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (PPRA);

Bibi Rose, Kaimu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma;

Wakili Bahame Nyanduga Mwenyekiti Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora;

Bw. Mathew Kirama, Mkurugenzi, Idara ya Ukuzaji wa Maadili, Ofisi ya Rais, (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora);

Viongozi mbalimbali wa Serikali;

Viongozi wa Dini;

Wageni waalikwa;

Waandishi wa Habari;

Mabibi na Mabwana:

ASALAAM ALEYKUM; BWANA ATUKUZWE!

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, kwa kutujalia uzima na kutuwezesha kukusanyika hapa leo ili kushiriki katika uzinduzi wa maadhimisho ya wiki ya kutoa huduma kwa Wananchi kama sehemu ya kuadhimisha Siku ya Maadili Kitaifa na Haki za Binadamu, uzinduzi ambao unaambatana na upokeaji wa kero na malalamiko ya Wananchi. Hii ni siku muhimu kwetu na kwa Taifa zima.

Niwashukuru pia wale wote waliofanikisha maandalizi haya kwa njia moja au nyingine. Kipekee nimshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) na wasaidizi wake, viongozi wa Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma,Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Utumishi wa Umma, Ofisi ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali (NAO), Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) na

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa jitihada zao kubwa za kuratibu na hatimaye kufanikisha uzinduzi huu wa siku ya maadhimisho ya siku ya maadili Kitaifa na Haki za Binadamu ulioambatana na utoaji huduma kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kupokea malalamiko yao. Hongereni sana!

Ndugu Wananchi, kama nilivyokwishadokeza, leo tunazindua wiki ya utoaji wa huduma na upokeaji wa malalamiko ya wananchi kama njia ya kuelekea kwenye maadhimisho ya Siku ya Maadili Kitaifa na Haki za Binadamu yatakayofanyika kitaifa tarehe 10 Desemba, yaani siku ya Jumamosi wiki hii. Kwa mara ya kwanza Kitaifa, tutakuwa tukiadhimisha siku hii kwa namna ya pekee ambapo Taasisi Saba zinaungana na kuratibu maadhimisho haya kwa pamoja. Hii, inatokana na ukweli kwamba Tanzania tumeazimia kuwa Taifa ambalo linazingatia misingi ya maadili, kupambana na rushwa na kukuza uzingatiaji wa Haki za Binadamu, Uwajibikaji na Utawala Bora.

Kauli mbiu ya kitaifa ya Siku ya Maadili Kitaifa na Haki za Binadamu mwaka huu ni “Kujenga na Kukuza Maadili, Haki za Binadamu, Uwajibikaji, Utawala Bora na Mapambano dhidi ya Rushwa” inayoakisi mambo ambayo kila mmoja wetu popote pale alipo na wakati wowote ule ana wajibu wa kuhakikisha kuwa Uadilifu na Haki za Binadamu zinatambuliwa, zinalindwa na kuheshimiwa.

Natumaini wote tutatafakari kauli mbiu hii ya “Kujenga na Kukuza Maadili, Haki za Binadamu, Uwajibikaji, Utawala Bora na Mapambano dhidi ya Rushwa” tukijikumbusha kuwa Maadili na Haki za Binadamu siyo anasa bali ni kitu muhimu katika maisha yetu sote, wanawake kwa wanaume, vijana kwa wazee, wasichana kwa wavulana, pamoja na watoto, wana haki ya kufurahia huduma bora zinazotolewa na Taasisi za Umma bila

kulazimika kutoa rushwa.

Ndugu Wananchi; kama nilivyogusia hapo awali, misingi iliyopo ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Mikataba ya Kimataifa na Kikanda ya Haki za Binadamu na Sheria mbalimbali za Nchi, inailazimu Serikali ya Tanzania kulinda na kukuza Maadili na Haki za Binadamu. Katika jitihada zake za kutimiza wajibu huu muhimu wa kulinda na kukuza Maadili na Haki za Binadamu, na kuhakikisha kuwa Maadili pamoja na mapambano dhidi ya rushwa yanaimarishwa, Serikali yetu imekwishaingiza baadhi ya mikataba hii katika Sheria zetu za Nchi, kwa kutunga Sheria mpya au kurekebisha zile zilizopo.

Ndugu Wananchi, utoaji wa huduma na upokeaji wa malalamiko ya Wananchi unatoa fursa nzuri kwetu sote kuwasilisha kero zetu mbalimbali ambazo zitafanyiwa kazi na vyombo vyetu vya Serikali ambavyo vina wajibu kisheria kusimamia haki za Wananchi. Maadhimisho ya Siku ya Maadili Kitaifa na Haki za Binadamu ni lazima yaende sambamba na ufanisi wa kazi zetu na utoaji huduma kwa jamii.

Serikali itaendelea kutimiza wajibu wake wa kuziwezesha Taasisi zinazosimamia Maadili, Mapambano dhidi ya Rushwa, Haki za Binadamu na Uwajibikaji ili ziweze kutimiza wajibu wake ipasavyo. Napenda kuwahakikishia kuwa, malalamiko ya kila Mwananchi yataheshimiwa na kufanyiwa kazi kwa wakati.

Ndugu Wananchi, pamoja na juhudi kubwa za Serikali za kuboresha mazingira ya upatikanaji wa huduma kwa Wananchi Nchini, natambua wapo watendaji wanaochelewesha utoaji wa huduma. Napenda kuwahakikishia kuwa Serikali ya Awamu ya

Tano imejipanga vyema kukabiliana na utendaji usioridhisha na bila kumwonea haya, huruma wala muhali mtu yeyote anayejihusisha na matumizi mabaya ya Ofisi, Madaraka, vitendo vya rushwa na uzembe kazini.

Ndugu Wananchi, Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imedhamiria kwa dhati kabisa kupambana na Rushwa na Ufisadi, Ukiukwaji wa Maadili na kutowajibika kwa Watumishi na Viongozi wa Umma.

Pia, Serikali itaendelea na mapambano dhidi ya ubadhirifu, wizi na ufujaji wa mali na fedha za Umma. Hata hivyo, yote haya yatafanikiwa ikiwa kila mmoja wetu atatekeleza wajibu wake kwa kuzingatia Maadili, Sheria, na kuheshimu Haki za Binadamu.

Ikumbukwe kwamba ubadhirifu, wizi, rushwa na ufisadi umechangia katika kudumaza ukuaji wa uchumi wa Nchi yetu na hivyo, kuendeleza hali ya umaskini wa Wananchi walio wengi, wakati wachache wakineemeka. Hali hiyo haikubaliki hata kidogo, kwani ikiachiwa iendelee, itarudisha nyuma jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano katika kufikia malengo ya Kimataifa ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals).

Ndugu Wananchi, nitumie fursa hii pia kuwaasa Watanzania wenzangu kuanzisha kampeni maalum za kukuza Maadili katika ngazi mbalimbali zikiwemo zile za Utumishi wa Umma, Taasisi za Dini, Taasisi za Elimu na katika nyanja zote za maisha ya kila siku. Suala hili likifanyika vizuri, naamini sote kwa pamoja, tutakuwa tumetimiza wajibu wetu wa kulinda Haki za Binadamu, kwani bila Maadili mema, itakuwa vigumu kuheshimu utu wa mwanadamu ambao ndio msingi mkuu wa haki za binadamu;

na hivyo kutekeleza kauli mbiu ya ‘Kujenga na Kukuza Maadili, Haki za Binadamu, Uwajibikaji, Utawala Bora na Mapambano dhidi ya Rushwa’.

Jukumu la kukuza, kulinda na kuheshimu Maadili na Haki za Binadamu ndani ya jamii yetu, ni letu sote, mtu mmoja mmoja, familia au kaya na Serikali kwa ujumla. Serikali ya Awamu ya Tano itaendelea kuhakikisha kuwa Maadili, Haki za Binadamu, mapambano dhidi ya rushwa na Misingi ya Utawala Bora inazingatiwa hapa nchini.

Ndugu Wananchi, nimedokezwa pia kuwa wiki hii ya kuwahudumia Wananchi kupitia mabanda yaliyopo hapa Mnazi Mmoja itakwenda sambamba na zoezi la kuchangia Damu kwa hiari, hivyo niwaalike Watumishi wa Umma na Wananchi kufika hapa Mnazi mmoja pamoja na kupata au kujifunza huduma zinazotolewa hapa na kutoa malalamiko yetu, tuhiari vilevile kutoa Damu ili kuwasidia Wananchi wenzetu walioko mahospitalini na kwingineko wanaohitaji huduma ya kuongezewa damu.

Baada ya kusema hayo, natamka kuwa maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu, ikiambatana na utoaji wa huduma na upokeaji wa malalamiko ya wananchi yamefunguliwa rasmi.

ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA.